Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF); Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF); Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF); Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA); na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA).

**2.2.1Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya OWM-KVAU**

**i. Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA)**

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ulianzishwa kupitia GN. 332/2001 ya Sheria ya Wakala za Serikali Namba 30 ya Mwaka 1997. Aidha, Utendaji kazi wa Wakala unasimamia utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi Namba 5 ya Mwaka 2003 (OSH Act. 2003) na Kanuni zake, Sera ya Taifa ya Afya na usalama mahali pa kazi 2010; na Mikataba na Miongozo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) inayosimamia masuala ya Usalama na Afya Mahali pa kazi.

**ii. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii awali lilianzishwa mwaka 1964 kama Idara ya Serikali chini ya Wizara ya Kazi, likawa Shirika kamili linalojitegemea mwaka 1975, na baadaye kubadilishwa kuwa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa Sheria Na. 28 ya mwaka 1997.

Shirika lina majukumu ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuwekeza katika miradi yenye kuleta faida na kuwezesha kulipa mafao bora kwa wanachama wake.

**iii. Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)**

Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ulianzishwa kupitia Sheria Namba 2 ya mwaka 2018 baada ya kuunganishwa kwa Mifuko minne ya (PSPF, LAPF, GEPF na PPF). Majukumu ya PSSSF ni pamoja na kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza katika miradi yenye kuleta faida na kutoa elimu kwa Umma.

**iv. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)**

Tume hii ilianzishwa mwaka 2007 kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 2004 ya Taasisi za Kazi. Tume ina majukumu ya kusuluhisha na inapolazimu kuamua juu ya migogoro ya kikazi.

KWA TAARIFA ZAIDI
SCAN QR CODE


Kwa Mawasiliano Zaidi:

**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**
**S.L.P 2890, DODOMA**
**TANZANIA**
**www.kazi.go.tz**
**ps@kazi.go.tz**


# IJUE OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU NA TAASISI ZAKE

## 1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (OWM - KVAU) imeanzishwa kwa Hati Idhini ya Serikali Na. 57A iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 24 Januari, 2022.

OWM-KVAU ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusu masuala ya Kazi, Vijana, Ajira, Watu Wenye Ulemavu na Hifadhi ya Jamii. Aidha, OWM - KVAU katika kufikia majukumu hayo inaongozwa na Dira na Dhima zifuatazo: -

**1.1 Dira**
Jamii yenye mahusiano mema mahali pa kazi, nguvukazi shindani na maisha bora.

**1.2 Dhima**
Kukuza fursa za ajira, viwango vya kazi, kinga ya jamii, majadiliano ya pamoja na kuwawezesha Vijana na Watu wenye Ulemavu.

## 2.0 MAJUKUMU YA MSINGI YA OWM - KVAU

Majukumu ya Msingi ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ni yafuatayo:-

i. Kusimamia Sheria za Kazi na kuratibu utekelezaji wa viwango vya kazi vya Kimataifa vinavyotolewa na Shirika la Kazi la Duniani (ILO);

ii. Kuratibu shughuli za Maendeleo ya Vijana ikiwa ni pamoja na kuhimiza masuala ya uzalendo na kujitegemea;

iii. Kuratibu uzalishaji wa Fursa za Ajira za Staha hususani kwa Vijana na Watu wenye Ulemavu;

iv. Kuratibu masuala ya Hifadhi na Kinga ya Jamii;

v. Kusimamia Mipango ya Kukuza Tija, Ubunifu na Ufanisi kazini;

vi. Kuratibu na Kusimamia Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu;

vii. Kusajili na Kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri;

viii. Kusimamia Masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi;

ix. Kuboresha Utendaji na Maendeleo ya Rasilimaliwatu; na

x. Kusimamia Taasisi zilizo chini ya OWM-KVAU.

## KIMUUNDO OWM – KVAU

OWM-KVAU inasisimamia Ofisi na Taasisi zifuatazo:-

### 2.1.1 Ofisi za Kazi za Mikoa

OWM-KVAU ina Ofisi za Kazi katika Mikoa yote 26 Tanzania Bara na Vituo maalumu vitano (EPZA, TIC, Mkuranga, Kinondoni na Makao Makuu). Vituo hivyo vilianzishwa kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi; kusimamia mahusiano mema sehemu za kazi; na kutaribu ajira za raia wa kigeni nchini.

### 2.1.2 Ofisi za Huduma za Ajira

Huduma za Ajira zinatolewa kupitia Ofisi zinazoratibiwa katika Kanda Nne (4) ambazo ni: Kanda ya Mashariki na Pwani inayohudumia Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani, Morogoro, Mbeya, Ruvuma, Songwe na Rukwa; Kanda ya Kaskazini inayohudumia Mikoa ya Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga na Manyara; Kanda ya Kati inayohudumia Mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa, Tabora, Kigoma na Katavi; na Kanda ya Ziwa inayojumuisha Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga, Geita, Mara na Simiyu.

Ofisi hizo pamoja na majukumu mengine huwaunganisha watafuta kazi na waajiri; kutoa mbinu bora za utafutaji kazi; kuratibu upatikanaji wa ajira za Watanzania nje ya nchi; na kuratibu Mafunzo ya Uzoefu Kazini kwa Wahitimu wa Vyuo ngazi mbalimbali (Internship Programme).

### 2.1.3 Vituo vya Maendeleo ya Vijana

Ofisi ina Vituo vya Maendeleo ya Vijana katika Mikoa Mitatu (3) ya Kilimanjaro (Marangu), Songwe (Sasanda - Mbozi) na Morogoro (Ilonga - Kilosa). Vituo hivyo vina jukumu la kuhamasisha na kutoa elimu kwa vijana kuhusu masuala ya ujasiri, kilimo, TEHAMA, ujasiri amali, uongozi, stadi za maisha na maadili.

### 2.1.4 Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu

OWM-KVAU ina Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu katika Mikoa Sita (6) ya Singida, Dar es Salaam, Tabora, Mwanza, Mtwara na Tanga ambavyo vinatoa mafunzo ya aina mbalimbali kwa wenye ulemavu.

## 2.2 Taasisi zilizo chini ya OWM – KVAU

Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inasimamia Taasisi Tano (5) ambazo ni: